# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA

**23 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA - TAREHE 23 MEI, 2025

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka

wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**388 MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA (MBINGA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Shule ya Sekondari ya Wasichana Mbinga itapandishwa hadhi kuwa ya Kidato cha Tano na Sita.

**389 MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati wa Shule Kongwe nchini.

**390 MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Shule za Msingi nchini kwa kuwa Shule nyingi ni chakavu.

**391 MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Vituo vya Afya vitajengwa Kata za Kilimalile, Mabale, Minziro, Mutukula, Ruzinga, Ruyango, Kitobo na Bugandika - Nkenge.

**OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

**392 MHESHIMIWA ROBERT CHACHA MABOTO (BUNDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, Serikali ina mpango gani kuwekeza kwenye eneo la EPZA katika Halmashauri ya Mji wa Bunda.

**WIZARA YA NISHATI:**

**393 MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa muda mfupi wa kuhakikisha Wananchi wa Vijijini wanatumia Nishati Safi ya kupikia badala ya Kuni na Mkaa.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**394 MHESHIMIWA BAHATI KENETH NDINGO (MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itajenga maeneo rasmi ya Uvuvi kwa ajili ya Wavuvi Wilayani Mbarali.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**395 MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti Tembo waliovamia Kata ya Engikaret - Longido ili kunusuru maisha ya Wananchi.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**396 MHESHIMIWA TUMAINI BRYCESON MAGESSA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, zoezi la uandikishaji wa Vitambulisho vya NIDA ni endelevu ukizingatia kila mwaka kuna Vijana wanaopata sifa ya kuandikishwa.

**WIZARA YA KILIMO:**

**397 MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, nini mkakati wa Serikali kutokomeza Magonjwa ya Michungwa Wilayani Kilwa.

**398 MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia Soko la uhakika Wananchi wa Wilaya ya Kyerwa wanaolima Zao la Vanila.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**399 MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEGE (MWIBARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itaondoa tatizo la upungufu wa vitabu vya kufundishia katika Shule za Sekondari - Mwibara.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**400 MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Kasanga utaanza pamoja na ukarabati wa Mahakama za Mwanzo Mwazye na Mwimbi.

**401 MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU (KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti utoaji holela wa Vyeti vya Vifo.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**DODOMA**
**23 MEI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**